**ZIARA>> Kukagua shughuli za udhibiti wa usafiri wa majini**

# TASAC yasisitiza usalama wa usafiri majini nchini

**Na NICHOLAOUS KINYARII (OUT)**

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), limeielekeza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), kuzingatia sheria na kanuni za usafiri majini.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TASAC, Nahodha Mussa Mandia, alisema hayo wilayani Mafia, mkoani Pwani, juzi wajumbe wa bodi hiyo walipofanya ziara ya ukaguzi wa shughuli za udhibiti wa usafiri wa majini.

Aliitaka TPA kufuata sheria na kanuni za usalama wa usafiri majini katika kutoa huduma Bandari ya Kilindoni, kisiwani Mafia.

"TASAC ni mdhibiti na kuna sheria na kanuni tunazisimamia, wenzetu TPA ni watekelezaji, inatubidi tuwakague mara kwa mara na kuwaelekeza wapi pa kurekebisha kuondoa kasoro hizi ndogo na hatarishi.

"Fikirieni kuwa na maboya ambayo ikitokea dharula mtu kutumbukia anarushiwa boya," alisema.

Aidha, alihimza ushirikiano baina ya taasisi nyingine hususan inapotokea dharula kwa kuwa suala la usalama ni jukumu la vyombo vyote vya serikali, wavuvi na wananchi.

Akikagua gati ya kuhudumia meli za abiria na mizigo, Mussa alibainisha gati hilo linahitaji ukarabati mkubwa kwa kuwa mbao zake zimelegea, nyavu za uzio wa pembeni mwa gati zimechanika na hakuna vifaa vya kujiokolea.

"Gati hili linahitaji ukarabati mkubwa kwa kuwa mbao zake zimelegea, nyavu za uzio wa pembeni mwa gati zimechanika na hakuna vifaa vya kujiokolea.

"Hivyo, wazamiaji mara inapotokea dharula inaweza kusababisha mtu au mizigo kutumbukia katika maji maana, kuna wakati hali ya bahari inakuwa siyo shwari," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa TASAC, Mohamed Salum alibainisha changamoto za Mafia ni nyingi na kuna maeneo wamebaini yanahitaji kuboreshwa kwa haraka ikiwemo kusogeza huduma zao karibu na wananchi kwa kuanzisha ofisi ndogo, kama ilivyo katika kisiwa cha Ukerewe, Ziwa Victoria.

Ofisa Msimamizi wa Bandari kutoka TPA, Ramadhan Mkango alisema licha ya kutoa huduma, bado kuna changamoto ya ukarabati wa gati na kuweka vifaa vya uokozi.

Aliishukuru Bodi ya Wakurugenzi TASAC kufika na kuahidi maelekezo yalitolewa watafanyia kazi, kuhakikisha usalama unaimarika wa kusafirisha abiria na mizigo.

Katibu wa Umoja wa Wavuvi Mafia, Mohamed Tego aliiomba TASAC kuimarisha usalama wa usafiri majini kwa kuwapatia vyombo vya uokozi, kusaidia kuokoa watu pale ajali za majini zinapotokea.

"Sisi wavuvi usiku na mchana tupo majini kutafuta riziki na huwa inatokea watu wanapata ajali na tunachanga na kwenda kuwatafuta, wakati mwingine wanapatikana na wengine wanapotea jumla na chombo. Lakini chombo kikiwepo ni rahisi kuwasha na kuelekea eneo la tukio kwa haraka," alisema.

Tego alisema Kisiwa cha Mafia kina samaki mkubwa duniani Papa Potwe ambaye ni kivutio cha utalii na kuiomba TASAC izielekeze meli zinapofika ukanda wa bahari eneo la Mafia zipunguze mwendo na kujiepusha na kuchafua mazingira, kuwalinda samaki hao na mazalia ya samaki wengine ambao ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Mafia.

Ziara hii ya wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi TASAC ilianza Julai 22, mwaka huu, katika Wilaya ya Mafia, itafutia Nyamisati, Bagamoyo na inatarajiwa kuhitimishwa Julai 27, mwaka huu, mwalo wa Mkwaja, mkoani Tanga.

**KONGAMANO**



**WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo (katikati) akiwa na viongozi wa Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI), kabla ya kufungua kongamano kuhusu dira ya taifa ya 2050 na kuzindua Tuzo za Rais kwa Mzalishaji Bora Viwandani (PMAYA) jijini Dar es Salaam, jana. (Na Mpigapicha Wetu).**

# e-GA, wadau wajadili mifumo ya teknolojia

**Na MWANDISHI WETU**

MAMLAKA ya Serikali Mtandao (e-GA), imekutana na wadau katika mwenendo wa kujengeana uelewa kuhusu matumizi ya mifumo ya teknolojia ya mawasiliano katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

Akizungumza baada ya kufungua mkutano huo, uliofanyika hivi karibuni, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Benedict Ndomba alieleza teknolojia mpya ya 'Blockchain' inafanya taarifa kudhibitiwa sehemu moja, hivyo kusaidia kila mtu katika mzunguko kuipata.

Mhandisi Ndomba alieleza kuwa, wamekutana kupata uelewa wa pamoja na taasisi za umma na mashirika yapo katika mifumo hiyo.

Alisema taasisi za umma zikitumia mfumo huo utawezesha huduma kuwa bora kutokana na taarifa kutodhibitiwa na mtu mmoja.

Pia, Mhandisi Ndomba alisema kuna mfumo mwingine wa sarafu za kidijiti utakaorahisisha namna ya kutoa huduma za kifedha na miamala katika taasisi za umma kwa kushirikiana na taasisi fedha zikiwemo benki.

Alibainisha kwamba, teknolojia za mawasiliano na mifumo ya teknolojia inabadilika, hiyo mamlaka hiyo lazima kwenda nayo kuhudumia taasisi za umma katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

"Kama Mamlaka lazima tuone mbali kuhusu mifumo ya mawasiliano katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma za mawasiliano na taasisi za umma bila kikwazo na huduma hizo wanapata kwa wakati," alisema.

Ndomba alisema katika teknolojia kutokuwa sehemu moja kutaondoa udanganyifu baadhi watoa huduma.

Aliendelea kusema e-GA wanaendelea kufanya utafiti kwenda na dunia na usalama wa teknolojia ya mawasiliano.

Mwenyekiti wa UABA, Yaliwe Mlambo alisema wameamua kushirikiana na Tanzania kutokana na kuwa mbele katika teknolojia ya mifumo.

Blockchain ni teknolojia ya kidijitali inayotumika kusimamia na kuhifadhi rekodi za shughuli za kielektroniki kwa njia ya uwazi, salama na isiyo na udhibiti wa mamlaka moja.

**USHIRIKIANO**

**MIFUMO**

Mwenyekiti wa UABA, Yaliwe Mlambo alisema wameamua kushirikiana na Tanzania kutokana na kuwa mbele katika teknolojia ya mifumo.

## CTI yatoa mapendekezo Dira ya Maendeleo 2050

**Na MWANDISHI WETU**

SHIRIKISHO la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), limependekeza maendeleo ya viwanda yapewe kipaumbele katika Dira ya Taifa ya 2050.

Mwenyekiti wa CTI, Leodegar Tenga alisema hayo jana, katika mkutano wa wadau wa viwanda kujadili Dira ya 2050 na kuzungumzia maendeleo ya viwanda kwa ujumla.

Mkutano huo ulioandaliwa na CTI, pia ulizindua tuzo za Rais za Mzalishaji Bora Viwandani PMAYA, ambazo hufanyika kila mwaka kwa wenye viwanda.

Tenga alieleza hakuna nchi duniani iliyowahi kupiga hatua kubwa kiuchumi, bila kuwekeza katika viwanda, hivyo lazima kuwe na mikakati madhubutu ya kukuza viwanda.

"Kuna msemo wa Kiswahili kwamba; kupanga ni kuchagua kwa hiyo tuchague kuwekeza katika viwanda tusonge mbele," alisema.

Alisisitiza viwanda vifanye kazi vizuri lazima serikali iwekeze pia katika ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli na rasilimali watu.

"Maono ya nchi ni kujipanga tutimize tulichopanga, kwa hiyo sisi CTI tunaamini viwanda ni muhimu na kupata rasilimali lazima tuwekeze pia katika kilimo.

"Tumefungua masoko mengi upande wa Afrika Mashariki (EAC), Kusini mwa Jangwa la Sahara (SADC), sasa tujipange kuuza bidhaa zetu za viwanda nje ya nchi, badala ya sisi kuwa soko la bidhaa za wenzetu," alisema.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji), Profesa Kitila Mkumbo alisema katika maandalizi ya Dira ya Taifa 2050 yameweka kipaumbele kikubwa katika maendeleo ya viwanda, nia ikiwa ni kuondoa utegemezi wa kununua bidhaa nyingi nje ya nchi.

Profesa Mkumbo alisema wasomi wamesema katika maandiko yao kuwa tofauti kubwa baina ya nchi tajiri na zile maskini ni kwamba nchi tajiri zina viwanda vingi, wakati zile maskini hazina viwanda na zinategemea kununua bidhaa nje ya nchi.

"Itakuwa vigumu kutengeneza Dira ya Taifa bila kuweka viwanda katikati ya dira hiyo, kwa sababu hilo ni la msingi na tafiti nyingi zinaonyesha hatuwezi kuendelea kwa kuendelea kununua bidhaa nje ya nchi, lazima tuwe na viwanda vingi tuuze nje," alisema.

Alisema katika utafiti uliofanywa na serikali katika maandalizi ya dira hiyo uliohusisha watu 7,668 nchi nzima waliochaguliwa kisayansi, walitaka vipaumbele vitano viwepo katika dira hiyo.

Alitaja miongoni mwa vipaumbele hivyo ni suala la viwanda na kwamba asilimia 65 ya malighafi zinazotumika viwandani zinatokana na kilimo, hivyo kilimo kitaendelea kuwa kipaumbele cha dira hiyo.

Kipaumbele kingine ni uwekezaji mkubwa katika rasilimali watu kwa kuwa uchumi wa viwanda unahitaji watu waliosoma vizuri.

"Lazima dira yetu ituelekeze kuwekeza katika elimu na siyo elimu tu, bali elimu iliyoborа," alisema.